

Mwongozo wa msingi wa uendelezaji wa vizazi

Uendelezaji wa vizazi ni nini?

Kwa urahisi, ni zoezi la kukuza mifugo. Kwa umaalum zaidi, ni sehemu ya sayansi ya wanyama inayotathmini thamani ya maumbile ya mifugo kwa kutumia uchambuzi unaojulikana kama utabiri bora wa ukoo usiokuwa na upendeleo.

Mchakato huu, ambao umeleta mapinduzi katika uzalishaji wa mifugo, huchagua wanyama wenye makadirio bora ya thamani ya uzalishaji katika ukuaji na uzalishaji au wenye sifa zinazopendelewa kwa ajili ya uzalishaji.

Njia za uendelezaji wa vizazi/Koo

Uzalishaji wa asili

Kawaida hujulikana kama huduma ya kila siku, njia hii hutumia dume kumuhudumia ng'ombe jike akiwa kwenye joto.

Hasara za uzalishaji wa asili

- Kusambaa kwa magonjwa ya zinaa kama vile kutupa mimba kwa magonjwa ya trikomoniasisi na vibriosisi.
- Ukosefu wa kumbukumbu huongeza uwezekano wa kuchanganya damu ya koo moja, matokeo yake ni ng'ombe dhaifu.
- Kukosekana kwa kumbukumbu ya afya za madume yasiyo bora ambayo hutumika kwa uzalishaji wa asili.
- Ni gharama kutunza dume kwa upande wa malisho, wafanyakazi na huduma za afya.
- Madume kilema hawawezi kutumika hata kama wana nguvu.
- Madume huwa na kikomo cha idadi ya ng'ombe jike wanaopanda nao kwa siku.
- Madume huweza kuwa na fujo na kuwa hatari kwa wafugaji na kaya zao.



Faida za uzalishaji wa asili

- Ugrunduzi wa joto wa uhakika
- Uwezekano mkubwa wa uzalishaji kwasababu ya idadi kubwa ya mbegu zinazolingia
- Urahisi wa gharama za uzalishaji wa asili.



Ng'ombe aina ya Friesian aliyeboreshwa akifurahia chakula chenye afya.

Koo, Rangi, Kiwango cha mafuta ya maziwa na kiwango cha uzalishaji wa maziwa

| Koo | Rangi | Nafasi kati- ka kiwango cha mafuta ya maziwa | Nafasi ka- tika uzalishaji wa maziwa |
|-----------|--------------------|---|--|
| Friesians | Nyeupe na Nyeusi | 4 | 1 |
| Ayrshire | Nyekundu na Nyeupe | 3 | 2 |
| Guernsey | Kahawia na Nyeupe | 2 | 3 |
| Jersey | Kahawia | 1 | 4 |

Uhimilishaji

Uhimilishaji ni utaratibu ambao mbegu huchukuliwa kutoka kwa dume, na kisha kuhifadhiwa na kupandikizwa ndani ya mfumo wa uzazi wa jike kwa lengo la kuzalisha. Mbinu ambayo hutumika mara kwa mara ni ile ya kupima kwa haja kubwa ambapo vifaa hutumika kuhimilisha. Mrija uliowekwa dawa huingiwa kwenye uke na huongozwa kwenye mfuko wa uzazi kwa njia ya kuingiza mkono wenye mpira kwenye njia ya kinyesi, kasha mbegu huwekwa na mhimilishaji mwisho wa mlango wa uzazi.

Faida za Uhimilishaji

- Inadhibiti kusambaa kwa magonjwa ya zinaa
- Huongeza kasi ya kuboresha vinasaba yaani kuboresha na kuongeza daraja la kundi bora.
- Huruhusu matumizi ya mbegu kutoka kwa dume hata baada ya dume kufa au kupata kilema.
- Dume mmoja anaweza kuhudumia majike wengi (zaidi ya majike 500000 kwa dume mmoja).
- Mbegu ya dume huhifadhika na kusafirishwa umbali mrefu kirahisi.
- Ni salama kwa wafugaji na kaya zao.

- Inawezesha usahihi na haraka usambazaji wa taarifa kuhusu vinasaba vya dume kwa wakulima na wahimilishaji.
- Inaruhusu wakulima kutunza kumbukumbu za vinasaba.

Hasara za uhimilishaji

- Gharama ya huduma ni ya juu.
- Inahitaji wafanyakazi wazoefu na gharama za vifaa ziko juu.
- Uwezekano wa kuchukuliana na utambuzi wa joto.

Dalili za Joto

- Kutoa ute kupitia uke.
- Kulia/kupiga kelele.
- Kuhangaika-Ng'ombe huwa na fujo na makini kuliko kawaida
- Kushuka kwa kiwango cha uzalishaji wa maziwa au maziwa kutotoka kabisa.
- Kupanda ng'ombe wenzie na kukubali kupandwa au kutulia anapopandwa.
- Kupotea kwa hamu ya kula
- Uke huvimba na kuwa mwekundu.

Sababu muhimu kwa wakulima kuzingatia watumiapo uhimilishaji kwa ajili ya uendelezaji wa vizazi/koo

1. Mkulima lazima aweke kumbukumbu ya kila ng'ombe.
2. Ng'ombe akiwa kwenye joto, mkulima amwite mhimilishaji mara moja na kumpa taarifa ya dalili za joto.
3. Mhimilishaji anapofika, lazima ajue dume waliopo na sifa zao ili mkulima asaidiwe katika kuchagua dume bora.
4. Ni muhimu kwa mkulima kuzingatia uchaguzi wa ng'ombe dume kwa kuangalia sifa kuliko kuangalia gharama ya mbegu dume.
5. Ni muhimu sana kupima mimba kwa kipindi kilichopangwa na mhimilishaji au bwana mifugo ili kujua kama ng'ombe ni mwenye mimba.

Sifa muhimu za kuzingatia wakati wa kuchagua dume

Orodha ya kipaumbele katika mpangilio wa muhimu

- Fomu ya maziwa
- Kina cha kiwele
- Urefu kiwele kwa nyuma
- Mpangilio wa chuchu
- Muunganiko wa kiwele kwa mbele
- Mgawanyiko wa kiwele
- Mwelekeo wa kwato na pembe

Sifa za uchambuzi wa dume

- Dume thabiti
- Uzalishaji wa maziwa
- Wingi na asilimia ya mafuta
- Protini na asilimia yake
- Upana wa kiwele kwa nyuma

